**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BENKI KUU YA TANZANIA**

**TAARIFA KWA UMMA**

# UZINDUZI WA KIELELEZO CHA FAIDA REJEA YA DHAMANA ZA SERIKALI (TANZANIA SOVEREIGN YIELD CURVE)

Benki Kuu ya Tanzania, kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inatangaza uzinduzi rasmi wa kielelezo cha faida rejea ya dhamana za serikali (Tanzania Sovereign Yield Curve), uliopangwa kufanyika siku ya Ijumaa, Tarehe 7 Agosti 2026, katika Ukumbi wa Benki Kuu ya Tanzania, Dar es Salaam, kuanzia saa 5:00 asubuhi hadi saa 7:00 mchana.

Hii ni hatua muhimu katika kuendeleza soko la ndani la dhamana za Serikali, ikitarajiwa kuleta uwazi sokoni, kuboresha upatikanaji wa bei halisi za soko, kuchochea ukuaji wa soko la upili, na kuweka msingi thabiti na wa kuaminika katika kupanga bei za dhamana za Serikali pamoja na bidhaa nyingine za kifedha.

Benki Kuu ya Tanzania inawakaribisha wadau mbalimbali wa sekta ya fedha, wakiwemo watoa elimu ya fedha pamoja na wawekezaji wote, kushiriki katika uzinduzi huu.

Unaweza kuhudhuria baada ya kuthibitishwa kupitia usajili wa njia ya mtandao kwa kuskani QR Code hapa chini, au kujiunga mubashara mtandaoni kupitia chaneli rasmi za mitandao ya kijamii za Benki Kuu ya Tanzania.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na Idara ya Masoko ya Ndani, Benki Kuu ya Tanzania, 2 Mtaa wa Mirambo, 11884, S.L.P 2939, Dar es Salaam; Simu: 2233530/3565/3527/3275; Barua pepe: info@bot.go.tz au botcommunications@bot.go.tz na Tovuti: www.bot.go.tz.